# MAJIBU KWA MASWALI KUHUSU SIKU YA PENTEKOSTE

**“Nanyi mtajihesabia tangu siku ya pili baada ya Sabato…. Hata siku ya hiyo Sabato ya saba mtajihesabia siku hamsini…. Nanyi mtapiga mbiu siku iyo hiyo kutakuwa na kusanyo takatifu kwenu” (Mambo ya Walawi 23:15, 16, 21).**

Bwana aliyefufuka aliwaambia wanafunzi wake, “Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini (Yerusalemu) hata mvikwe uwezo utokao juu” (Luka 24:49). Chanzo na kusudi ya uwezo huo inatolewa wazi katika kitabu cha matendo: Lakini mtapokea uwezo mtakapovikwa na *Roho Mtakatifu*; na *mtakuwa mashahidi kwangu* katika Yerusalemu, na katika Yudea yote na Samaria, hadi mwisho wa dunia” (Matendo 2:8).

Ahadi ya Baba ilikuwa Roho Mtakatifu, itakayowavika na kuwahimiza walipoenenda kufanya kazi waliyopewa na Yesu. Kama mashahidi kwa mwokozi aliyefufuka, wanafunzi walipaswa “kuihubiri injili kwa kila kiumbe” (Marko 16:15) na kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi wakiwabatiza… [na] kuwafunza kushika yote Yesu aliwaamuru (Mathayo 28:19-20). Lakini hawatakuwa na uwezo wa kufanya kazi Yake kwa nguvu zao wenyewe. Walihitaji uwezo – uwezo kutoka juu. Walihitaji Roho Mtakatifu kuwaongoza, kuwafunza, kuwahimiza, na kufanya ndani yao kuhakisha ulimwengu wa dhambi na haki, na hukumu (Yohana 16:8-15).

Roho iliwajilia jinsi Yesu alivyosema. Siku ambayo Roho ilikuja ilikuwa siku spesheli; siku ya kwanza ya mfumo jipya katika mpango wa Mungu wa ukombozi. Siku hiyo ilikuwa *siku ya Pentekoste.*

Hebu tuwe makini kwa siku hii muhimu ya kitakatifu, tuelewe maana yake ya kiasili, kile maadiko yanasema kuihusu, na maana yake kwa Wakristo wa kisasa. Njia moja bora ya kusoma somo ni kuigawa somo lenyewe katika mada tofauti; na kuchunguza kila mada kupitia maswali. Maswali yajayo na majibu na majibu yanapaswa kuwasaidia watu waliyo wageni kwa siku takatifu waweze kuelewa vizuri maana ya Pentekoste, na (kwa matarajio) kutoa uchunguzi mwafaka kwa wale ambao wamekuwa wakitazama sherehe za kila mwaka kwa miaka mingi.

**Pentekoste inapatikana wapi katika Agano la Kale**?

Neno *Pentekoste* halipatikani katika Agano la kale, lakini siku takatifu itakayojulikana kwa jina hilo linapatikano hapo. Neno lina asili ya Kigiriki na humaanisha “ya hamsini.” Siku hiyo takatifu inakuja katika siku ya hamsini – tangu siku hiyo mganda wa sadaka hutikiswa (Mambo ya Walawi 23:15-21). Katika Agano la Kale, sherehe huitwa “Siku Kuu ya Majuma” (Kutoka 34:22); inayosimamia masiku saba ya “siku kuu ya mavuno” na siku ya malimbuko (Hesabu 28:26).

**Sherehe ilimaanisha nini kwa Israeli ya kale?**

Siku kuu ya majuma ilikuwa sherehe ya kushukuru. Wanaume wa Israeli, pamoja na familia zao, na watumwa, na vile vile Walawi, wajane, mayatima, na wageni wanaokaa kwa ardhi yao, walipaswa kufurahia mbele zake BWANA katika siku kuu ya majuma (Kumbukumbu la Torati 16:11). Kwa maneno mengine, walipaswa kuja mbele zake Bwana kwa kushukuru ili mavuno yabarikiwe kwa yale Aliyowafanyia.

Walipaswa kukumbuka kwamba walikuwa watumwa kule Misri: (aya ya 12). Wakikumbuka mapitio hayo iliwahimiza kuwarehemu watumwa, maskini, na wageni (wakijumuisha Wamisri) waliokaa nao.

Siku kuu ya Majuma iliwakumbusha Waisraeli zile kanuni za Mungu. Mungu aliahidi kwamba ikiwa wate wangezitii amri zake, atawabariki. "Utabarikiwa uzao wa tumbo lako, na uzao wa nchi yako, na uzao wa wanyama wako, wa mifugo, maongeo ya ng'ombe yako, na wadogo wa kondoo zako…. Bwana ataiamuru baraka ije juu yako katika ghala zako na mambo yote utakayotia mkono wako, nayo atakubariki katika nchi akupayo Bwana…. Bwana atakufanya uwe na wingi wa uheri, katika uzao wa tumbo lako, na uzao wa wanyama wako wa mifugo, na uzao wan chi yako, katika nchi BWANA aliyowaapia Baba zako kwamba atakupa. Atakufunulia Bwana hazina yake nzuri, nayo ni mbingu, kwa kutoa mvua ya nchi yako kwa wakati wake, na kwa kubarikia kazi yote ya mkono wako" Kumbukumbu la Torati 28:4, 8, 11, 12).

**Sherehe hii inamaanisha nini kwa Kanisa la Agano Jipya?**

Hebu kwanza tuchunguze kanuni zilizotumiwa katika Agano la Kale. Mungu alisema, "Hapo mtakapokuwa mmekwisha ingia hiyo nchi niwapayo, na kuyavuna mavuno yake, ndipo mtakapomletea kuhani mganda wa *malimbuko* ya mavuno yenu; naye atautikisa mganda mbele za Bwana ili kwamba ukubaliwe kwa ajili yenu; siku ya pili baada ya Sabato kuhani atautikisa" (Mambo ya Walawi 23:10-11).

Mganda wa malimbuko ulipaswa kutikiswa siku ya jumapili ("siku baada ya Sabato"). Kama vile Masadukayo, Wasamaria na wengine wakati wa Kristo, tunachukua hili kumaanisha Jumapili ya mkate usiotiwa chachu.

Sasa, hebu tuchunguze Agano Jipya.
Paulo anaandika, "Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, *limbuko* lao waliolala. Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu, kadhalika na kiyama cha wafu ililetwa na mtu. Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa. Lakini kila mmoja mahali pake; *limbuko* ni Kristo; baadaye walio wake Kristo, atakapokuja" (1 Wakorintho 15:20-23).

Kristo aliwasilishwa hai mbele zake Mungu asubuhi ile mganda wa malimbuko ulitikiswa. Wakati Mariamu Magdalene alimtambua asubuhi hiyo, alimwambia, "Usinishike, kwa maana

sijapaa kwenda kwa Baba. Lakini enenda kwa ndugu zangu ukawaambie, ‘Ninapaa kwenda kwa Baba Yangu, naye ni Baba yenu, kwa Mungu Wangu, naye ni Mungu Wenu”’ (Yohana 20:17).

Ishara haina makosa. Mganda wa malimbuko hutoa picha ya Kristo *wazi* na kuwasilishwa kwake akiwa hai mbele za Baba.

Lakini kumbuka, kutikisa maganda wa malimbuko hutokea siku ya kwanza ya mavuno ya majuma saba (Mambo ya Walawi 23:15). Siku baada ya Sabato ya majuma saba ndiyo Siku Kuu ya Majuma (aya ya 16).

Tazama kinachotokea siku hiyo:
“Mtatoa katika mazao yenu mikate miwili ya kutikiswa, itakuwa ya sehemu za kumi mbili za efa; itakuwa ya unga mwembamba, itaokwa na chachu, iwe *malimbuko* kwa Bwana…. Kisha kuhani atawatikisa pamoja na hiyo mikate ya *malimbuko* kuwa sadaka ya kutikiswa mbele za Bwana… Nanyi mtapiga mbiu siku iyo hiyo; kutakuwa na kusanyo takatifu kwenu; msifanye kazi yoyote ya utumishi…” (Mambo ya Walawi 23:17, 20, 21).

Sasa hebu turudi katika Agano Jipya.
Yakobo anaandika, “Kwa kupenda kwake menyewe alituzaa sisi kwa neno la kweli, tuwe [sisi Wakristo] kama *limbuko* la viumbe vyake” Yakobo 1:18. Yakobo anasema juu ya “jeshi la kanisa” au kanisa katika ulimwengu huu. Na katika Ufunuo 14 wale 144,00 “walionunuliwa katika nchi” na wamfuatao “Mwana-Kondoo kila aendako” wanaitwa “*malimbuko* kwa Mungu na kwa Mwana-Kondoo” (aya ya 3-4). Hii ndio picha iliyotabiriwa ya kanisa iliyotukuzwa.

Ikiwa mganda wa malimbuko uliotikiswa siku ya kwanza ya mavuno inawakilisha Kristo kama limbuko la kwanza, basi mikate iliyotikiswa lazima iwakilishe kanisa – “limbuko la kwanza kwa viumbe vyake.” Na kwa kuwa mganda uliotikiswa unawakilisha Kristo katika utukufu wake wa ufufuo, mikate iliyotikiswa inawakilisha sio tu kanisa la kisasa bali pia “ushindi wa kanisa” au kanisa katika utukufu wake wa ufufuo. Majuma saba ya mavuno kati ya mikate iliyotikiswa inatukumbusha juu ya mavuno yanayoendelea ya maisha kwa ufalme wa Mungu – kazi ya kusanya malimbuko “kwa wakati utakaowasilishwa hai mbele zake Baba kama Kristo aliye limbuko letu la kwanza alivyowakilishwa.

Kwetu, Siku Kuu ya Majuma – au siku ya Pentekoste – ni ukumbusho wa ujio wa Roho Mtakatifu (Matendo 2) na ukumbusho wa kutia motisha  kwa utukufu wetu ujao. Pia ni ukumbusho wa kila mwaka kwa jukumu letu la “kuishi katika Roho” (Wagalatia 5:25), “kuenenda katika Roho” (aya ya 16, 25), “kuongozwa kwa Roho” (aya ya 18), kutoa “tunda ya Roho” (aya ya 22-23), na “kutozimisha Roho” (Wathesalonike 5:19).

**Mbona hamtazami Pentekoste katika siku ya kalenda ya Sivani 6?**

Tunaamini maelekezo ya kiasili ya kuhesabu siku ya Pentekoste inahitaji kutikisa mganda wa malimbuko siku ya Jumapili. Hiyo huweka Siku ya Pentekoste – siku hamsini baadaye – siku ya

Jumapili. Hesabu ya siku hamsini huanzika kwa Jumapili ya Mkate Usiotiwa Chachu. Lakini kutokea mwaka hadi mwaka, Jumapili hiyo hutokea kwa wakati tofauti kati ya sherehe. Kwa hivyo Siku ya Pentekoste inayotokea siku hamsini baadaye mara zote huwa siku ya Jumapili katika tarehe tofauti za kalenda.

Wasomi wametoa hoja katika pande zote za mjadala. Tunaamini kwamba uchunguzi mufti wa ushahidi wa pande zote ni kwa niaba ya Pentekoste Jumapili.

Kwanza maneno ya maandiko yenyewe huunga mkono maoni hiyo: "Nanyi mtajihesabia tangu siku ya pili ya Sabato, tangu siku hiyo mliyouleta mganda wa sadaka ya kutikiswa; zitatimia sabato saba; hata siku ya pili ya hiyo Sabato ya saba mtajihesabia siku hamsini…" (Mambo ya Walawi 23:15-16).

Tazama kwamba kuhesabu huanza siku baada ya Sabato, kisha Sabato saba hupita, na kuisha siku baada ya Sabato ya saba. Kwetu, hatuoni utata hapa. Siku baada ya Sabato ni Jumapili. Hesabu siku hamsini kishe umalize kwa Jumapili inayofuatilia. Kama hiyo sio wazi, tunaambiwa kwamba siku ya hamsini ni siku baada ya Sabato ya saba. Hiyo itakuwa Jumapili!

Lakini wawakilishaji wa Sivani ya 6 hawaridhiki kwa hiyo kuelewa rahisi wa neno *Sabato.* Wanadai kwamba "Sabato" ya kwanza hapa ni siku takatifu ya kwanza ya Sherehe ya Mkate Usiotiwa Chachu – Sabato ya kila mwaka. Wanadai tena kwamba "Sabato" zilizo kati ya siku hiyo na Pentekoste sio *siku* za Sabato bali ni "majuma" – vipindi saba mfululizo zinazohusisha siku saba kila mmoja – ambavyo vinaweza au haviwezi kuisha kwa sabato. Ikiwa tutachukua "Sabato saba" kumaanisha "majuma saba," na "Sabato ya saba" kumaanisha "juma ya saba" basi mbona hatuchukui "siku baada ya Sabato" kumaanisha "siku baada ya wiki"? Ikichukuliwa hivyo, tunaweza kufikiria ya kwamba "siku baada ya wiki" humaanisha siku baada ya wiki iitwayo Sherehe ya Mkate Usiotiwa Chachu. Ni sherehe ya *siku saba* (Mambo ya Walawi 23:6-8), na maelekezo ya kuhesabu Pentekoste huja tu baada ya aya chache za kutajwa kwa "siku ya saba" ya sherehe hii, ambayo ni Sabato ya kila mwaka na mwisho wa kipindi cha siku saba maalum (tazama aya ya 8-11).

Lakini tukichukuwa "Sabato" (Kiebrania: *Shabbat*) katika maana yake, basi hitimisho la kimantiki ni kuwa "siku baada ya Sabato" humaanisha siku baada ya sabato ya kila *wiki* – Jumapili!

Andiko la pili linatoa tarehe za kalenda ya Pasaka, siku za kwanza na za mwisho ya Mkate Usiotiwa Chachu, Sikukuu ya tarumbeta, Siku ya Upatanisho, na siku ya kwanza ya Sikukuu ya Vibanda, lakini sio kwa Siku ya Pentekoste. Hii huonekana kutowezekana, hasa ikiwa siku hii ilikuwa (kama rabi wa baadaye walivyodai) ukumbusho wa kutoa sheria kule Sinai. Huenda sheria ilitolewa katika Sika ya Pentekoste, lakini maandiko hayasemi hivyo. Wasomi wengine wanaamini kwamba tarehe ya kalenda iliyowekwa ya Pentekoste ilianzishwa *baada ya* rabi kuanza kutazama siku hili takatifu kama ukumbusho wa utoaji wa sheria.

Ya tatu, maandiko hutuelekeza *kujihesabia* hadi siku ya Pentekoste. Ushahidi huu ingawa haujitolei uamuzi, kwamba Pentekoste ya kiasili haikutokea tarehe fulani ya kalenda lakini ilihesabiwa kutoka kwa siku iliyoweza kutokea wakati wowote ndani ya Siku za Mkate Usiotiwa Chachu.

Hizi ndizo hoja za kimsingi zaidi zinazokumbatia Pentekoste ya Jumapili, lakini kuna ushahidi zaidi. (Ikiwa unahitaji somo la ziada kuhusu mada hii, tuandikie au tupigie simu kwa nakala yako ya bure ya kijitabu, *Je! Tunapaswa kutazama Pentekoste katika Sivani ya 6?*)

**Mbona mnajihesabia kutoka kwa Jumapili ya Mkate Usiotiwa Chachu badala ya Sabato ya kila wiki inayotokea ndani ya Siku za Mkate Usiotiwa Chachu?**

Biblia haisemi kwamba kujihesabia siku hamsini inapaswa kuanza wakati wa au karibu na Sherehe ya Mkate Usiotiwa Chachu. Ingawa Mafarisayo na Masadukayo walitazama kanuni tofauti za kuhesabu, walianza kuhesabu ndani ya Sherehe ya Mkate Usiotiwa Chachu, na wengine walionekana kuanza kujihesabia siki *baada ya* sherehe, ingawa walitumia kalenda tofauti na ile iliyotumiwa na Mafarisayo na Masadukayo. Tamaduni hizi zinazo shina la kawaida: Zote huunganisha hesabu ya kutikisa mganda hadi Pentekoste pamoja na Sherehe ya Mkate Usiotiwa Chachu. Kipengele cha kawaida huonekana kuashiria kusudi la maelekezo ya kiasili. Kwa maneno mengine, inaonekana kwamba Mungu alikusudia kwamba hesabu ya siku hamsini kiunganishe Mkate Usiotiwa Chachu pamoja na Pentekoste.

Lakini hata hivyo, swali bado linasimama. Tunapaswa kuanza kujihesabia kwa Jumapili inayotokea ndani ya Mkate Usiotiwa Chachu? Au tunapaswa kuanza kwa Sabato ya kila wiki inayotokea ndani ya sherehe? Kwa kuwa Maandiko hayasemi hivyo, mmoja lazima afanye uamuzi juu ya kule cha kufanya.

Kunazo sababu za kiteolojia kwa kuanza kujihesabia hadi Pentekoste na Jumapili inayotokea ndani ya Mkate Usiotiwa Chachu. Kristo alifufuliwa kutoka wafu na kuwakilishwa hai mbele za Baba wakati wa Sherehe ya Mkate Usiotiwa Chachu. Sherehe inatoa picha ya Kristo kama “Mkate wa Maisha” tunayemtegemea kwa maisha ya kiroho. Inaonekana kimantiki kwamba siku hiyo hutoa picha ya Kristo kama Malimbuko wa mavuno wa kiroho ya Mungu itakayotokea *ndani ya* sherehe ambayo kwa nguvu huashiria kazi Yake ya ukombozi.

Umuhimu mwingine ni uwezekano kwamba Masadukayo, Wasamaria, na wengine waliotazama Pentekoste ya Jumapili walianza kujihesabia kwa Jumapili ndani ya Siku za Mkate Usiotiwa Chachu. Hiki ndicho tolea la kumi na moja ya *Encyclopaedia Britannica* kinasema: “Malimbuko yanapaswa kusanywa siku ‘baada ya Sabato’ (Lev. Xxxiii. II). Kifungu hiki kimejenga mada ya utata kati ya Wasamaria na vitengo vingine na wayahudi [k.v Mafarisayo], ya kwanza waliochukulia kwamba *uliashiria Jumapili ya kwanza wakati wa sherehe*, na ya mwisho kama kama ishara maalum kwa siku ya pili ya sherehe yenyewe…” (Vol. 20. Article: “Passover,” p. 889, emphasis added).

**Kanisa lilitazama Pentekoste ya Jumatatu hadi 1974. Mbona ulibadilishwa?**

Kitambo kabla ya mabadiliko haya kufanywa, wachungaji na waamini walikuwa na shaka kuhusu jinsi kanisa lilivyoamua tarehe ya Pentekoste. Mnamo 1974, mada ulichunguzwa tena na matokeo yalikuwa mabadiliko jinsi kanisa lilivyohesabu masiku yaliyoongoza Pentekoste.

Mambo ya Walawi 23:15 inasema tunapaswa kujihesabia "*kutokea* siku ya pili baada ya sabato." Ilijailiwa kwamba "kutokea" ilimaanisha *"mbali na,"* inayoonelea kuhesabu kwa kutohusisha badala ya kuhusisha.

Suluhisho la kosa linajumuisha kusoma vizuri Mambo ya Walawi 23:15-16. Kujihesabia huanza *kutokea* siku baada ya Sabato, *hadi* siku ya Sabato ya saba, jumla ya siku hamsini. Maandishi yenyewe yanasisitiza kwamba kujihesabia (*Kutokea* Jumapili hadi Jumapili ni sawa na siku hamsini) hujumuisha. Kwa maneno mengine, inajumuisha ile "siku ya kwanza baada ya Sabato." Ukianzia siku ya Jumapili na kuhesabu siku hamsini, siku ya hamsini itakuwa Jumapili. (Kumbuka kwamba neno *Pentekoste* humaanisha *"ya hamsini.")* Siku ya "hamsini na moja" haijarejelewa, na hakuna uwezekano kwamba Siku ya Pentekoste ni siku baada ya siku hamsini.

**Je! Kanisa la kwanza la Agano Jipya liliendelea kutazama Siku ya Pentekoste katika miaka zilizofuatilia ujio wa kwanza wa Roho Mtakatifu?**

Ndio. Wanafunzi wa kwanza wa Yesu walikuwa Wayahudi, na Siku ya Pentekoste ilikuwa ya muhimu kwa Wayahudi wote. Kwa wanafunzi, ilikuwa muhimu zaidi wakati wa ujio wa Roho Mtakatifu siku hiyo (Matendo 2). Ilichukua maana ya muhimu zaidi. Kuepuka sherehe muhimu kama hiyo haikuwezekana.

Kwa kuongezea Matendo 2, Maandiko mengine mawili ya Agano Jipya yanataja Pentekoste. Ya kwanza ni Matendo 20:16: "Kwa sababu Paulo alikusudia kupita Efeso merikebuni, asije akakawia katika Asia; kwa maana alikuwa na haraka akitaka kuwahi Yerusalemu Siku ya Pentekoste kama ikiwezekana." Ya pili ni 1 Wakorintho 16:18: "Lakini nitakaa Efeso hata Pentekoste," asema Paulo.

Zikijisimamia, maandishi haya hayahitimishi ushahidi kwamba Wakristo wa awali walitazama siku ya Pentekoste. Lakini ukweli kwamba Paulo anataja Pentekoste kwa Mataifa waliobadilika inaonyesha wazi kuwa walikuwa wakiifahamu na kuitazama.

Rekodi ya kihistoria inaonyesha bila shaka kwamba kanisa la awali lilitazama Siku ya Pentekoste. Njia ya kuitazama ilibadilishwa kwa wakati lakini wengi wa wanateolijia wa kwanza na watetezi za haki walitaja Pentekoste kama sherehe la Kikristo. Haiwezekani kabisa kwamba wanateolojia wa karne ya pili siku moja walianza kuitazama Pentekoste. Bila shaka, mazoezi yao yalitoka kwa kanisa la awali la Apostolic.